**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUGAJI NYUKI - TABORA

# TANGAZO LA MAFUNZO YA MUDA MFUPI

Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora kinapenda kuwajulisha kuwa Kutakuwa na Mafunzo ya ufugaji Nyuki ya muda mfupi (Short course) yatakayo endeshwa chuoni mwezi Septemba, 2025. Kozi hii imelenga kutoa elimu ya kitaalamu kwa watu binafsi, vikundi vya vijana, wanawake, wakulima, na wajasiriamali wanaopenda kuanza au kuboresha shughuli za ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuongeza kipato na kulinda mazingira.

## MADA ZITAKAZOTOLEWA NI PAMOJA NA:

i. Aina, makundi na tabia za nyuki
ii. Uanzishaji na utunzaji wa manzuki za Nyuki wanaodunga
iii. Uanzishaji na utunzaji wa manzuki za Nyuki wasiodunga
iv. Sera na miongozo ya ufugaji Nyuki
v. Zana za kisasa za ufugaji Nyuki
vi. Mazao yatokanayo na nyuki
vii. Mbinu bora za uvunaji, uchakataji na ufungashaji wa mazao ya nyuki
viii. Viwango na ubora wa mazao ya nyuki
ix. Kuongeza thamani katika mazao ya nyuki.

## MUDA NA ENEO LA MAFUNZO

- Muda wa mafunzo ni siku tano (5), kuanzia tarehe 8 hadi 12 Septemba 2025
- **Mahala:** Ukumbi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora.

## GHARAMA ZA MAFUNZO

Kila mshiriki anatakiwa kugharamia Tsh. 500,000 kwa ajili ya:

- Mahitaji ya mafunzo ya nadharia na vitendo
- Ziara fupi,
- Cheti cha ushiriki,
- Kifungua kinywa na Chakula cha mchana kwa kipindi chote cha mafunzo.

## NJIA YA MALIPO

⇨ Malipo yanafanyika kwa njia ya mfumo wa serikali (Control Number) utakayopatiwa kutoka chuoni.

⇨ Lipia gharama ya mafunzo kujihakikishia nafasi yako.

**HUDUMA ZA MALAZI: Washiriki watakuwa huru kujitafutia huduma za malazi.**

- Ndani ya chuo kuna huduma ya malazi kwa gharama ya Tsh. 5,000 kwa siku.
- Pia maeneo ya jirani na chuo unaweza kupata nyumba za kulala wageni kwa gharama kati ya Tsh. 10,000 na 20,000.
- Aidha, kwa manispaa ya Tabora kuna aina mbalimbali za majengo ya kulala wageni.

**MAWASILIANO KWA AJILI YA UFAFANUZI, KUJIANDIKISHA NA KULIPIA**

- Wasiliana nasi kwa simu namba **+255 766315078** au barua pepe **info@bti.ac.tz**.
- Au tembelea ofisi za chuo zilizopo Tabora mjini barabara iendayo airport.
- Tuma maombi yako mapema ili kujihakikisha nafasi yako.
    - ⇨ ***Chuo chetu kimejikita katika kutoa elimu bora na yenye viwango vya kitaifa na kimataifa ili kusaidia maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini. Tunatoa wito kwa wananchi wote kutumia fursa hii adimu kwa manufaa binafsi, familia, jamii na taifa kwa ujumla.***

**~~~NYOTE MNAKARIBISHWA~~~**

**Imetolewa na:**
Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora.
**19 Juni, 2025**